hatua kali ikiwa ni pamoja na kutozwa faini zinachu-

"Lengo la ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Njombe ni kukiwezesha

zoainisha na Mheshimiwa Mbunge hazitakuwepo tena," ilieleza.

# Vyama vya wavuvi vyapata bil 2.6/-

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi kupitia Dawati la Sekta Binafsi imeviunganisha vyama vya ushirika vya wavuvi na taasisi za fedha ambapo mpaka sasa mikopo iliyoombwa na kupitishwa ni Sh bilioni 2.6.

Hayo yalibainishwa na wizara hiyo wakati wa kujibu swali la msingi la Mbunge wa Mpanda Vijijini, Moshi Kakoso (CCM).

Akiuliza swali lake bungeni jana, Kakoso aliyetaka kujua mpango wa serikali wa kuwasaidia wavuvi wadogo kupata zana za kisasa ili kuondoa changamoto ya kushindwa kuvuna rasimali za Ziwa Tanganyika lenye kina kirefu sana.

Majibu ya wizara kwa swali hilo yamebainisha kuwa serikali imetoa kipaumbele kwa sekta ya uvuvi ili iwapatie wananchi wake ajira, lishe, kipato na kuchangia katika Pato la Taifa kwa kuweka mazingira mazuri kwa wavuvi kupata mikopo ya masharti na riba nafuu kutoka katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo na kupitia Dirisha la Kilimo katika Benki ya Rasilimali (TIB).

Aidha, wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi imeviunganisha vyama vya ushirika vya wavuvi na taasisi za fedha ambako mikopo iliyoombwa na kupitishwa ni Sh bilioni 2.6 na mikopo iliotolewa ni Sh milioni 323.8.

Pia, wizara imehamasisha Benki ya Posta (Tanzania Postal Bank -TPB) kuzindua Akaunti ya Wavuvi kwa ajili ya mikopo na bima mahususi kwa wavuvi hususani wavuvi wadogo.

"Serikali pia imefuta Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye injini za kupachika, nyuzi za kushonea nyavu, nyavu za uvuvi na vifungashio kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2011 na Sheria ya Mamlaka ya Mapato (VAT Act) ya mwaka 2014 ili kuwasaidia wavuvi kupata zana za uvuvi kwa bei nafuu," ilieleza.

Pia serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wavuvi kufanya uvuvi wenye tija na kuwahimiza wavuvi kujiunga katika vikundi na kuanzisha vyama vya ushirika vya msingi, vyama vya akiba na mikopo (SACCOS) na Vicoba ili wakopesheke kwa urahisi na taasisi za fedha na hivyo kujikwamua kiuchumi.

"Serikali inahamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya kutengeneza boti na zana bora za uvuvi ili kuwezesha wavuvi kuzipata kwa bei nafuu na kwa urahisi," ilieleza.

Scanned with CamScanner

Wananchi wa Zanzibar wakiwa kwenye msururu wa kutoa pesa katika mashine ya ATM ya Benki ya Watu wa Zanzibar eneo la Darajani kutokana na uchache wa mashine hizo mjini humo hivi karibuni. (Picha na Martin Kabemba).

# Wavuvi kufunga pweza wazaliane zaidi

WAVUVI wa Kijiji cha Marumbi na Uroa wanakusudia kuanza kufunga na kufungua Pweza maeneo ya mwambao huo kuwawezesha kupata mavuno zaidi kwa wakati mmoja.

Mkuu wa diko la uvuvi la Kijiji cha Marumbi Wilaya ya Kati, Soud Abdallah alisema wanakusudia kuzungumza na majirani zao Kijiji cha Uroa kuweka utaratibu wa kufunga na kufungua uvuvi wa Pweza wavune wengi zaidi.

Alisema wamevutiwa na wavuvi wa Rasi ya Michamvi Wilaya ya Kati ambao mwezi Aprili walifungua uvuvi wa Pweza baada ya kufungia kwa miezi mitatu na kupata mavuno mengi.

"Tunakusudia kuanza kuweka utaratibu wa kufunga na kufungua uvuvi wa Pweza kwa muda wa miezi mitatu ili kuwawezesha wavuvi kupata mavuno na kipato kikubwa,"alisema.

Mvuvi wa Pweza katika kijiji cha Marumbi Mwajuma Punguza alisema utaratibu huo ni mzuri ambao miaka 10 ulikuwa ukitumika na kusaidia kuwawezesha kupata kipato kikubwa.

"Utaratibu huu tunaukaribisha, utatusaidia sisi wavuvi wa Pweza kupata kipato kikubwa, hivyo kusaidia shughuli zetu za maendeleo,"alisema.

Mkuu wa Hifadhi ya Minai kanda ya Wilaya ya Kati Unguja, Mohamed Ussi alisema utaratibu wa kufungia uvuvi wa Pweza miezi mitatu ni mzuri ambao hutoa nafasi ya kukua kwa viumbe hao na wavuvi kupata kipato kikubwa zaidi.

"Tumekubaliana kufungia uvuvi wa Pweza kwa miezi mitatu ili kutoa nafasi ya ukuaji na wavuvi kupata kipato kikubwa zaidi,"alisema.

Wavuvi wa kijiji cha Michamvi Wilaya ya Kati mwezi uliopita waliruhusu wavuvi kuvuna Pweza baada ya kuzuia uvuaji wake kwa zaidi ya miezi mitatu na kujipatia kipato kikubwa.

Utaratibu wa kufungia uvuvi wa Pweza hutolewa kwa miezi mitatu ambapo wavuvi hawatakiwi kuvua au kufanya shughuli zozote katika eneo lililotengwa lenye matumbawe na mwamba wenye mawe ambayo ndiyo makazi ya Pweza huku uvuvi wake ni wa ya kuchokoa.



Scanned with CamScanner

Meneja wa Tawi la Benki ya Stanbic Tanzania Mbeya, Hemedi Sabuni (wa tano kushoto), akikabidhi matangi na vitakasa kwa Ofisa Uchumi wa Halmashauri ya Mbeya, Saad Ahmad Mtambule (wa nne kulia) katika ofisi za halmashauri jana. Benki hiyo imetoa msaada huo ikiwa ni mchango wake katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa COVID-19. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wavuvi wapania kupata mavuno zaidi ya pweza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAVUVI wa Kijiji cha Marumbi na Uroa wanakusudia kuanzisha utaratibu wa kufunga na kufungua pweza katika maeneo ya mwambao huo ili kuwawezesha kupata mavuno mengi kwa wakati mmoja.

Mkuu wa diko la uvuvi la kijiji cha Marumbi Wilaya ya Kati, Soud Abdallah, alisema wanakusudia kuzungumza na majirani zao kijiji cha Uroa kuweka utaratibu wa kufunga na kufungua pweza kwa ajili ya kuwawezesha kupata mavuno mengi.

Alisema wamevutiwa na wavuvi wa rasi ya Michamvi Wilaya ya Kati ambao mwezi uliopita walifungua uvuvi wa pweza, baada ya kufunga kwa zaidi ya miezi mitatu na kupata mavuno mengi.

"Tunakusudia kuanza kuweka utaratibu wa kufunga na kufungua uvuvi wa pweza kwa miezi mitatu ili kuwawezesha wavuvi kupata mavuno mengi na kujipatia kipato kikubwa," alisema.

Mvuvi wa pweza katika kijiji cha Marumbi, Mwajuma Punguza, alisema utaratibu huo ni mzuri ambao zaidi ya miaka kumi ulikuwa ukitumika na kusaidia kuwawezesha kupata kipato kikubwa.

"Utaratibu huu tunaukaribisha kwa sababu utatusaidia sisi wavuvi wa pweza kupata kipato kikubwa na hivyo kusaidia kufanya shughuli zetu za maendeleo," alisema.

Mkuu wa Hifadhi ya Minai Kanda ya Wilaya ya Kati Unguja, Mohamed Ussi, alisema utaratibu wa kufungia uvuvi wa pweza kwa miezi mitatu ni mzuri ambao hutowa nafasi ya kukua kwa viumbe hao na wavuvi kupata kipato kikubwa.

"Tumekubaliana wakati wowote tunatarajia kutangaza kufunga uvuvi wa pweza kwa miezi mitatu ili kutoa nafasi ya ukuaji wake na hatimaye wavuvi kupata kipato kikubwa wakati wa uvunaji wake," alisema.

Wavuvi wa Kijiji cha Michamvi Wilaya ya Kati mwezi uliopita, waliruhusu wavuvi kuvuna pweza baada ya kuzuia uvuaji wake kwa zaidi ya miezi mitatu na kujipatia kipato kikubwa.

Utaratibu wa kufungia uvuvi wa pweza hufanyika kwa miezi mitatu, ambapo wavuvi hawatakiwi kuvua au kufanya shughuli zozote katika eneo lililotengwa lenye matumbawe na mwamba wenye mawe ambayo ndiyo makazi ya pweza.

Scanned with CamScanner